**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025

**JUNI, 2024**

# YALIYOMO

A. UTANGULIZI ........................................................................ 1
B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.......................... 4
C. UPATIKANAJI WA FEDHA............................................. 5
D. MAFANIKIO YA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024........................................................ 5
Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji.......................................................... 5
Programu ya Maendeleo ya Vijana.................................. 11
Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. ........................................................ 19
Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ............................ 29
Programu ya Uendeshaji na Mipango Katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo................ 30
E. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025........................................................ 36
F. PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKADIRIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 40
Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji........................................................ 41
i. Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari; na ................................................ 42
ii. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari,Utangazaji na Uchapaji........................ 42
Programu Kuu ya Maendeleo ya Vijana ............... 44
i. Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana........... 44
Programu Kuu ya Maendeleo ya Utamaduni,

Sanaa na Michezo. .................................................... 45
i. Programu Ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa; na .......... 46
ii. Programu Ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo. .................................................... 46
Progromu Kuu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo .................................................... 48
i. Programu Ndogo ya Uratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara; .......................... 48
ii. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; na .................................................... 48
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. .................................................... 48
G. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.................................................... 49
i. MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO .................................................... 49
ii. MAOMBI YA FEDHA 2024/2025............................ 50
I. MWISHO .................................................... 51
VIAMBATANISHO .................................................... 53

**HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO, MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kutushauri na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujalia kufika hapa tukiwa na afya njema na furaha. Namuomba Allah (S.W) aendelee kutudumisha katika amani na utulivu nchini kwetu. Atuzidishie imani thabiti ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ili kufikia maendeleo yaliyokusudiwa.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umahiri wake wa kuiongoza nchi yetu na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa majukumu ya Ilani ya Chama cha

Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 na Mipango Mikuu ya Kitaifa.

4. **Mheshimiwa Spika,** moyo wa kujitolea kwa hali na mali na uadilifu wa Dk. Mwinyi katika uongozi wake ni miongoni mwa mambo yanayoimarisha uwajibikaji na kuharakisha maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar. Namuomba Mwenye Mungu amzidishie hekima na busara katika kuwatumikia wananchi, ili tuendelee kufaidika na uongozi uliotukuka.

5. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais kwa namna walivyojitoa katika kuwahudumia wazanzibari. Nimefurahi kufanya kazi chini yao na ninawasihi wazanzibari kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia wasaidizi hawa waandamizi wa Mheshimiwa Rais ambao ni makini na wenye mapenzi ya dhati kwa nchi yao. Tuendelee kwa pamoja kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee kuwa na afya njema, hekima na busara katika kazi zao za kumsaidia Kiongozi Mkuu wa nchi.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kusimamia muhimili huu wa Baraza la Wawakilishi kwa umahiri mkubwa sana.

Aidha, ninakupongeza pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuongoza vyema majadiliano ya Bajeti za Wizara mbali mbali.

7. **Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa naomba nitumie fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mahiri na Mchapa kazi Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani, Makamo Mwenyekiti Mheshimiwa Nassor Jazira na Wajumbe wa Kamati kwa maoni, ushauri na mapendekezo mazuri waliyotupatia wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2024/25. Nakiri kwamba,mimi binafsi na watendaji wa Wizara yangu na Taasisi zake tumejifunza mambo mengi mazuri kutokana na hoja na ushauri wa Kamati hii.

8. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, napenda nitumie fursa hii, kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote wa Serikali ya awamu ya nane kwa kusimamia majukumu ya Wizara zao vizuri na kupelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020 - 2025.

9. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti, Makamo Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi

kwa ushauri na maelekezo wanayoyatoa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa ufanisi katika Serikali ya awamu ya nane.

10. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba uniruhusu niwasilishe kwa ufupi utekelezaji wa Programu za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kipindi cha Julai – Machi 2023/2024.

## B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, imetekeleza Programu kuu nne na programu ndogo nane chini ya Fungu J03. Programu Kuu hizo ni kama zifuatazo:

    **i.** Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji;

    **ii.** Programu ya Maendeleo ya Vijana;

    **iii.** Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

    **iv.** Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

## C. UPATIKANAJI WA FEDHA

*12.* **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilitengewa jumla ya **shilingi 51,939,984,000/-.** Kati ya hizo **shilingi 17,661,930,000/-** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 34,278,054,000/-** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Wizara iliingiziwa jumla ya **shilingi 44,226,110,342/-** sawa na **asilimia 85.** Kati ya hizo **shilingi 12,516,503,470/-** sawa na **asilimia 71** kwa kazi za kawaida na **shilingi 31,709,606,872/-** sawa na **asilimia 93** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. ***Kiambatisho nambari 1A kinahusika.***

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, Wizara ilipangiwa kukusanya **shilingi 875,997,000/-** na hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imefanikiwa kukusanya **shilingi 487,612,740/-** sawa na **asilimia 56. Kiambatisho no 1B na 1C kinahusika.**

## D. MAFANIKIO YA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

14. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 9,612,311,000/-** kwa

matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Programu hii iliingiziwa jumla ya **shilingi bilioni 7,326,462,894/-** sawa na **asilimia 76** kwa matumizi ya kazi za kawaida. ***kiambatisho namba 1A kinahusika.***

15. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imewawezesha wananchi wa ndani na nje ya Zanzibar kupata habari mbalimbali zikiwemo za utekelezaji wa Sera na Mipango ya Kitaifa inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwapatia Maendeleo wananchi wake.

16. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio yaliyopatikana kupitia programu hii ni pamoja na kuandika na kusambaza taarifa **866** za kijamii, kisiasa na kiuchumi na kusambazwa kupitia vituo vya habari vya umma na binafsi. Sambamba na Uuzaji wa picha za Viongozi Wakuu wa nchi **277** (picha **85** za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, picha **152** za Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na picha **40** za Rais Wastaafu).

17. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya UNESCO na Shirika la Habari la Internews iliandaa mafunzo maalum ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Maafisa Habari na Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jumla ya Maafisa 80 (Unguja 60

na Pemba 20) waliweza kunufaika na mafunzo hayo. Vile vile, Maafisa 25 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waliweza kushiriki mafunzo yaliyoandaliwa na Chama Cha Maafisa Habari na Mawasiliano Tanzania, mwezi Febuari 2024 Jijini Dar-es-Salaam.

18. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Studio za Redio la Shirika laUtangazaji Zanzibar lililopo RahaLeo unaendelea kutekelezwa kwa fedha za wahisani kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Lengo la mradi huo ni kuliboresha kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Mradi ulianza mwezi Febuari, 2024 na unatarajiwa kukamilika Julai, 2024 na unatarajiwa kugharimu jumla ya **shilingi 9,565,198,000/-**

19. **Mheshimiwa Spika,** miradi mengine iliyotekelezwa ni ununuzi wa vifaa vya kisasa vya studio, kufanya matengenezo ya studio za ZBC radio na Spice Fm Radio na kutengezaseti tano za ZBC TV kwa lengo la kuimarisha na kubadilisha muonekano wa ZBC. Maboreshohayo yamegharimiwa na fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

20. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii umeiwezesha ZBC kuandaa vipindi **10,900** kupitia TV, vipindi **7,194** kupitia Redio na vipindi **2,346** kupitia Spice FM. Sambamba na utayarishaji na

urushaji wa matangazo mbalimbali **20,837** na matangazo ya moja kwa moja **297.** Vile vile, Shirika la Utangazaji Zanzibar limefanikiwa kuanzisha vipindi vipya vikiwemo tabasamu, chapuo, karakana, kigoda na usiku wa lala unono.

**21.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata habari na taarifa za Serikali na nyenginezo kwa uhakika, Shirika la Magazeti ya Serikali limefanikiwa kuchapisha nakala **942,000** za magazeti, nakala **7,000** za Jarida la "Neema Zetu" na kutoa matangazo 2,647. Aidha, Shirika limeendelea kuboresha huduma zake. Kwa usambazaji wa habari na kujitangaza kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na website ya Shirika www.smsz.co.tz.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika programu hii, mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeiimarisha Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui kwa kukamilisha ujenzi mdogo wa ofisi kwa ajili ya kupunguza changamoto ya ufinyu wa nafasi, kufanya ukarabati wa duka la kuhudumia wateja lililopo Mkoroshoni, Chake chake Pemba na kuipatia kampuni Gari 1 kwa ajili ya matumizi ya kazi za ofisi.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeidhamini Kampuni ya ZMUX mkopo wa shilingi Bilioni Nne na Milioni Mia Tano

(**TZS 4,500,000,000/-**) ili kutekeleza mpango mpya wa Uwekezaji. Kupitia mpango huo Kampuni itaboresha Miundombinu ya kurushia matangazo, kufanya mageuzi ya kimfumo na ubora wa maudhui yatakayowezesha kuipatia faida na kutoa gawio Serikalini. Kwa sasa, Kampuni imekamilisha taratibu za upatikanaji wa Mshauri elekezi na mratibu wa mradi ambao watasimamia utekelezaji wa mradi huo utakaoanza mapema mwaka 2024/2025.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2024, Serikali imefanikiwa kutoa vibali **19** vya uchukuaji wa picha za kutengenezea filamu kwa makampuni mbali mbali ya ndani na njeya nchi, kibali 1 kwa Wakala wa habari na kusajili vijarida 3 navyo ni Zanzibar Investment and Business Insight (ZiBi) kutoka Kampuni ya Mwanana Communiction Limited, Zanzibar Kwanza kutoka Ofisi Kuu ya CCM Zanzibar na MWANASHERIA kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar. Lengo ni kudhibiti na kusimamia shughuli za Utangazaji kupitia sera na sheria za Habari na Utangazaji.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** mikakati mengine ya kudhibiti na kusimamia shughuli za utangazaji ni kufanya ukaguzi wa vituo vya utangazaji kwa kuhakikisha vinafuata masharti waliyopewa kwa mujibu wa leseni zao. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya vituo 59 (45 Unguja na 14

Pemba) vimefikiwa. Vituo 4 vya redio za FM vimechukuliwa hatua za kisheria baada ya kugundulika kwamba havifuati matumizi sahihi ya masafa waliyopangiwa. Pia, vituo 27 vya redio vimefanyiwa ufuatiliaji wa maudhui ili kuhakikisha maadili na masharti ya leseni za utangazaji yanafuatwa ipasavyo. ***Kiambatisho nambari 2A kinahusika.***

*26.* **Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine yaliyopatikana ni utoaji wa leseni 12 za vituo vya Utangazaji Unguja na Pemba kikiwemo kituo cha Televisheni cha DSTV, leseni saba (7) za maudhui ya mtandaoni na leseni nne (4) za vituo vya redio za FM.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa kazi za Serikali na binafsi zinachapishwa kwa ubora mkubwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji umepokea kazi za uchapaji **701** zenye thamani ya **shilingi Bilioni 2,052,475,126/**. Aidha, Magazeti Rasmi ya Serikali 41 yamechapishwa na kutangazwa kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Vile vile, mitihani ya kidato cha pili, darasa la saba na darasa la nne ya Baraza la Mitihani Zanzibar imechapishwa kwa ufanisi, usiri na kuwasilisha kazi hiyo kwa wakati.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala umefanikiwa kuongeza idadi ya mitambo ya uchapaji baada

ya kuifanyia matengenezo mitambo 2 ambayo ilikuwa na uchakavu wamudamrefu kwa kutumia mafundi wa ndani kutengeneza mitambo hiyo. Mitambo iliyofanyiwa matengenezo ni:- Four - Colour Sakurai na Stiching Machine.

29. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji unaendelea kutoa huduma za Bohari Kuu ya vifaa vya ofisini na kuandikia kwa taasisi za Serikali na binafsi. Jumla ya maombi **173** yenye thamani ya **shilingi milioni 104,142,435/-** yalipokelewa na kupatiwa huduma.

**Programu ya Maendeleo ya Vijana.**

***30.*** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 628,598,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2024 imeingiziwa jumla ya **shilingi 366,750,066/-** sawa na asilimia 58 kwa matumizi ya kazi za kawaida. ***Kiambatisho namba 1A kinahusika.***

31. **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mafanikio yaliyofikiwa kutokana na utekelezaji wa Programu hii ni Wizara kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005 na kuizindua Sera mpya ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2023, katika uzinduzi huo Mgeni rasmi alikuwa Makamo wa Pili wa Rais wa

Zanzibar Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah ambapo zaidi ya vijana 500 kutoka Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo, asasi zakiraia na vijana wenyewe walishiriki. Hatua hiyo muhimu inalenga kuimarisha mazingira bora ya Kisera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Kitaifa inayohusiana na ustawi na Maendeleo ya Vijana Nchini. Nawapongeza wadau wa Maendeleo ya Vijana hususan UNFPA kwa kushirikiana nasi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kukamilika kwa sera hii.

32. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la UNFPA imeanza maandalizi ya ***"Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Vijana Zanzibar 2025 – 2030"*** ili kusaidia utekelezaji wa Sera na kutoa muongozo kwa wadau juu ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo ya Vijana Nchini. Hatua iliyofikiwa ni kuajiri Mshauri elekezi, kuendesha vikao vya wataalamu pamoja na mikutano ya kukusanya maoni. Mpango huo unatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2024/2025. Vile vile, Wizara imekamilisha Muongozo wa Kitaifa wa Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya skuli, sambamba na kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa Kitaifa 21 (13 wanawake na 8 wanaume) kutoka taasisi za Vijana katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Muongozo huo utasaidia kuimarisha malezi na makuzi ya vijana nchini.

33. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuratibu na kusimamia utowaji wa mafunzo vijana **319,465** (196,688 Unguja na 122,777 Pemba) wakiwemo wanawake 172,981 na wanaume 146,484. Mafunzo yaliyotolewa ni ya Ujasiriamali, Stadi za Maisha, Afya ya Uzazi, elimu ya Uongozi na Uzalendo, mafunzo ya ushiriki na ushirikishwaji wa vijana, mafunzo ya amani na usalama, mabadiliko ya tabia ya nchi na mafunzo ya TEHAMA. Mafunzo haya yamewawezesha vijana kuchangamkia fursa zilizopo, kujitambua wao wenyewe na kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaisha.

*34.* **Mheshimiwa Spika,** kupitia sekta ya vijana, jumla ya **shilingi 212,611,431/-** na Vifaa vya uzalishaji vyenye thamani ya **shilingi 86,402,000/-** vimetolewa kwa vikundi 330na vijana mmoja mmoja 200 (117 Unguja na 83 Pemba). Msaada huo unatokana na jitihada kubwa za Serikali kupitia washirika wa Maendeleo ya vijana wenye lengo la kuwawezesha vijana ili waweze kujiendeleza kiuchumi. Maelezo kuhusu vikundi vilivyopatiwa msaada angalia ***Kiambatisho nambari 3C kinahusika.***

35. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ya Vijana Nchini (UNFPA, UNDP na EAC) ilifanikiwa

kuwasafirisha vijana watano na kiongozi mmoja. Vijana hao waliweza kushiriki katika mkutano wa mtandao wa vijana wa Afrika 2023 uliofanyika nchini Kenya, Mafunzo ya Amani na Usalama yaliyofanyika nchini Uganda na Mkutano wa Usimamizi wa Mradi wa Vijana (SYP) uliofanyika nchini Botswana.

36. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi za vijana na Mashirika ya Maendeleo nchini yakiwemo UNFPA na UNICEF huadhimisha siku ya Vijana Kimataifa ifikapo tarehe 12 Agosti ya kila mwaka. Kwa mwaka 2023 siku ya vijana ilifanyika uwanja wa Maisara na kuwashirikisha vijana kutoka makundi mbalimbali ikiwemo mabaraza ya vijana, Taasisi za Elimu, Asasi za kiraia, Vyama vya siasa, vijana wenye ulemavu na wawakilishi wa vijana kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba. Mgeni rasmi wa maadhimisho hayo alikuwa Mheshimiwa **Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.** Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa ***''Elimu na Ujuzi wa Kijani kwa Vijana na Maendeleo Endelevu ya Taifa''.*** Maadhimisho hayo yalitanguliwa na shughuli za usafi wa mazingira, makongamano na mabonanza ya michezo.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba vijana wanaunganishwa vyema na fursa

mbali mbali na kupata taarifa za uwezeshwaji, Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa mikopo kwa vijana ili waweze kujiimarisha kiuchumi na kujitegemea. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya vikundi **24** vya vijana (15 Unguja na 9 Pemba) vimewasilisha maombi ya mikopo kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) ambapo kati ya hivyo, vikundi **6** vimeshapatiwa mikopo yenye thamani ya **shillingi Milioni 62,000,000/-** na vikundi 18 vipo kwenye hatua wa kukamilisha taratibu za maombi ili waweze kupatiwa mikopo hiyo. Taarifa za vikundi hivyo zimeelezwa kwenye***kiambatisho nambari 3B kinahusika.***

***38.*** **Mheshimiwa Spika,** shughuli nyengine iliyotekelezwa kwa mafanikio makubwa ni kuvitembelea vikundi **349** vya kiuchumi (281 Unguja na 68 Pemba) vikiwemo vikundi **147** vya kuweka na kukopa. Lengo la ziara hizo ni kuvipatia ushauri wa kitaalamu, mafunzo ya uhamasishaji na kuwaunganisha na fursa mbalimbali za uwezeshaji. Aidha, Vikundi **96** vipya vya kiuchumi (81 Unguja na 15 Pemba) vimeanzishwa, vimesajiliwa na kuunganishwa na fursa za mikopo. Taarifa za vikundi hivyo zimeelezwa kwenye ***kiambatisho nambari 3A kinahusika***

**39.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, vijana **79** (46 wanawake na 33 wanaume) Pemba na

vijana **726** (382 wanawake na 344 wanaume) Unguja wamepatiwa mafunzo kupitia Vituo vya Mafunzo ya Vijana (YTC) viliopo Bweleo Unguja na Weni Pemba. Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha vijana wanapata stadi za maisha na kupambana na changamoto za utandawazi zinazowakabili, ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu sahihi za stadi za maisha na stadi za kazi. Mafunzo yanayotolewa ni pamoja na ushoni, TEHAMA, stadi za maisha, uongozi na ujasiriamali.

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na WatuWenye Ulemavu Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa. Kwa mwaka 2023 Mbio za Mwenge zilitumika kuwahamasisha wananchi hususan vijana kushiriki katika shughuli za maendeleo, mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/ UKIMWI, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, mapambano dhidi ya rushwa, ukatili dhidi ya binaadamu, Lishe Bora na mapambano dhidi ya Malaria.

41. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya miradi **1,424** yenye thamani ya **Shilingi trilioni 5.287/-** iliwekewa mawe ya msingi na mengine kuzinduliwa. Kwa upande wa Zanzibar miradi 53 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 158.999/-** ilizinduliwa na

mengine kuekewa mawe ya msingi. Vile vile, jumla ya lita 3,679 za damu salama zilichangiwa ambazo zitatumika katika hospital mbali mbali nchini. Aidha, kwa mwaka 2023, kilele cha Mbio za Mwenge wa uhuru kilifanyika tarehe 14 Oktoba, 2023 Mkoani Manyara na Kauli mbiu ya mwaka huo ilikuwa ***"Tunza mazingira, okoa vyanzo vya maji kwa ustawi wa viumbe hai na uchumi wa taifa".*** Vile vile, kwa mwaka huu wa 2024, mbio za Mwenge wa uhuru zimezinduliwa rasmi tarehe 2 Aprili katika Mkoa wa Kilimanjaro ukiwa na Kauli Mbiu isemayo:- ***"Tunza mazingira na Shiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ujenzi wa Taifa Endelevu".***

**42.** **Mheshimiwa Spika,** jumla ya vijana **1,979** wameweza kuhamasishwa na kushiriki katika shughuli mbalimbali za Kitaifa kwa lengola kuwajenga moyo wa kuwa wazalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao. Aidha, Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi ya SOS limefanikiwa kuandaa makala inayozungumzia shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Baraza la Vijana Zanzibar kwa lengo la kuwavutia vijana kujiunga na Baraza, kuwafanya kuwa wazalendo na kuipenda nchi yao pamoja na kulitambulisha Baraza kwa vijana wote wa Zanzibar.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kuzindua mpango mkakati

(Strategic Plan) wa Baraza la Vijana Zanzibar wa mwaka 2023-2028 ili kusaidia utekelezaji mzuri wa kazi za Baraza la vijana. Aidha, Baraza limefanikiwa kuwapatia mafunzo wafanya kazi 3 kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza kazi zao kwa mujibu wa sheria na kanuni za kazi.

44. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha shughuli mbalimbali za Baraza la Vijana Zanzibar, Baraza limefanikiwa kuanzisha Makala ya Baraza (Documentary). Lengo ni kutangaza kazi za Baraza kiuchumi pamoja na huduma zinazotolewa na vijana wa baraza la vijana. Aidha, Baraza limefanikiwa kuongeza idadi ya wanachama katika baraza la vijana kutoka 21,818 na kufikia 22,673 wakiwemo wanawake 10,206 na wanaume 12,467 ni sawa na ongezeko la wanachama 855.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Baraza la Vijana Zanzibar, jumla ya **shilingi 31,000,000/-** zimetumika katika kuyasaidia mabaraza ya vijana ngazi za Wilaya na shehia kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli zao. Vile vile, Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kusaidia shughuli za kiuchumi za vijana kwa kuwapatia vifaa vikundi vya shehia 8 za Pemba na shehia 14 za Unguja.

**Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.**

***46.*** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 38,256,150,000/-** kati ya hizo **shilingi 3,878,096,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 34,278,054,000/-** kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Wizara imeingiziwa jumla ya **shilingi 34,599,779,972/-** sawa na asilimia 90 kati ya hizo **shilingi 2,508,104,296/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na **asilimia 65** na **shilingi 31,709,606,872/-** sawa na **asilimia 92.5** kwa miradi ya Maendeleo. ***kiambatisho nambari 1A kinahusika.***

**47.** **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza na kuendeleza Utamaduni wa Mzanzibari, Programu hii iliwezesha kufanyika kwa Tamasha la 28 la Utamaduni wa Mzanzibari ambapo Shughuli mbali mbali zenye mnasaba na tamasha hilo zilifanyika ikiwemo maonyesho ya vyakula na madawa ya asili, sanaa za ngoma na maonyesho pamoja na paredi ya wasanii na wajasiriamali iliyosheheni vionjo vya kitamaduni. Zaidi ya wajasiriamali **74** na vikundi **56** vya sanaakutoka Unguja na Pemba vilishiriki. Vile vile, matamasha ya kijamii yakiwemo Tamasha la Mwaka Kogwa, ZIFF na Tamasha la Sauti za Busara yalifanyika. Lengo la matamasha hayo

ni kuhamasisha jamii kuendeleza, kulinda na kurithisha mila, silka, maadili na Utamaduni wa Mzanzibari.

48. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na muingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali na kuwepo kwa utandawazi kumepelekea jamii ya kizanzibari hususan vijana kuiga tamaduniza kigeni na kutokuthamini utamaduni wao. Serikali inaendelea kuchukuwa juhudi kubwaza kuwaelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuendeleza sanaa na utamaduni wa nyumbani. Sambamba na kuwataka wazazi na walezi kila mmoja kwa nafasi yake kushiriki kikamilifu katika kuwaelimisha watoto na vijana ili waweze kutambua na kufuata mila, silka na utamaduni wao.

49. **Mheshimiwa Spika,** maafisa 4 kutoka Idara ya Utamaduni Zanzibar waliweza kushiriki katika kikao muhimu cha urithi wa harakati za ukombozi kilichofanyika Dodoma tarehe 4 hadi 9 Machi, 2024. Ajenda zilizojadiliwa ni pamoja na kufanya uteuzi wa orodha ya Kitaifa ya urithi wa utamaduni usioshikika kulingana na vigezo mahususi. Kikao kiliazimia kufanya utafiti wa maeneo mapya yaliyopendekezwa ili hatimae yaingizwe katika orodha ya Kitaifa. Kadhalika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imefanikiwa kukisafirisha kikundi cha sanaa ya ngoma kushiriki katika tamasha la mambo ya

utamaduni wa India lililofanyika nchini India katika sherehe za uhuru wa nchi hiyo. Tamasha hilo lilifanyika kuanzia tarehe 2 hadi 18 Febuari 2024.

***50.*** **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, jumla ya kazi za sanaa **300** (17 sanaa za maonyesho na 283 filamu) zimekaguliwa na kufanyiwa uhakiki kwa ajili ya kutolewa makosa na maelekezo ili ziweze kutumika hadharani. Kati ya hizo kazi 5 hazikuruhusiwa kuoneshwa hadharani kutokana na kukiuka mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari. Vile vile, jumla ya taasisi **66** zimefanyiwa ukaguzi maalum kwa lengo la kuhakiksha wamiliki wanatii (comply) masharti ya sheria ya BASSFU na kanuni zake. Serikali inaendelea kuchukuwa juhudi kubwa ya kutoa elimu na kuhamasisha wasanii kuuenzi utamaduni wa mzanzibari, kulinda mila na silka, kushiriki matukio ya Kitaifa, kudumisha amani na uzalendo nchini. ***Kiambatisho nambari 4B kinahusika.***

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari kupitia Barazala Sanaaimefanikiwa kuanzishaprogramu ya kutoa tunzo kwa wasanii wanaofanya vizuri katika tasnia ya muziki. Tunzo hiyo imeanzishwa mwaka 2023/2024 na imepewa jina la **"Tunzo za Kimataifa za muziki Zanzibar" .** Aidha programu hii imewashirikisha wasanii wa nchi za Afrika Mashariki ambapo jumla ya wasanii

565 walishiriki katika kinyang'anyiro cha kuomba tunzo katika vipengele 29 vya aina mbali za muziki. Muziki wa Taarab asilia na nyimbo za utamaduni zilikuwa ni miongoni mwa vipengele vilivyoshindaniwa kwa ajili ya kuzienzi na kuziendeleza sanaa zetu hizi za asili ambazo zimeitangaza vizuri nchi yetu duniani kwetu. Tunawashukuru wadau wote mliotuunga mkono katika kufanikisha programu hii wakiwemoBenki ya Watu wa Zanzibar, ZURA, ZBC, na KENDWA ROCKS HOTEL.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, jumla ya wasanii **17** na vikundi **50** vya sanaa na utamaduni vimesajiliwa upya kwa ajili ya kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria namba 7 ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni ya mwaka 2015. Aidha, shughuli nyengine ambayo imetekelezwa ni kufanya ziara maalum ya kuwatembelea na kuwafariji wasanii wakongwe wa maigizo kwa kuwapatia sabuni na iftari katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Hatua hiyo inaashiria Serikali bado inawajali na kuthamini michango yao katika tasnia ya sanaa.

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuimarisha ushirikiano wa kikazi kati ya Baraza la Sanaa Zanzibar na Taasisi nyengine nje ya Zanzibar ikiwemo Baraza la Sanaa la Taifa, Bodi ya Filamu ya Tanzania na Kamisheni ya Filamu ya Kenya. Katika mashirikiano hayo Baraza

limeendelea kuimarisha programu za ukuzaji wa kazi za Sanaa, Programu ya uibuaji wa vipaji, uuandaaji wa tunzo na ubunifu wa kazi za Sanaa. vile vile, Baraza la Sanaa Zanzibar kwa kushirikiana na Bodi ya filamu Tanzania chini ya ufadhili wa Shirika la TIKA la Uturuki lipo katika mpango wa kuanzisha programu ya mafunzo ya ujengaji uwezo wa uzalishaji na Uongozi wa filamu, uainishaji wa maeneo ya filamu (Locations) na Uimarishaji wa masoko yafilamu.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Barazala Kiswahili Zanzibar imefanikiwa kufanya mafunzo ya Ufundishaji Kiswahili kwa Wageni kwa wahitimu wa Shahada ya Kwanza, walimu wa Sekondari na wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili ambapo jumla ya washiriki **101** wamehitimu mafunzo hayo. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu na mbinu za ufundishaji lugha ya pili ili waweze kuzitumia fursa za kusomesha Kiswahili ndani na nje ya nchi.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ikishirikiana na Wizara ya Utamaduni na Sanaa ya Tanzania Bara imefanikisha kufanya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani yaliyofanyika tarehe 7/7/2023 ambapo kwa Tanzania kilele cha Maadhimisho hayo kilifanyika

Zanzibar. Watu mashuhuri kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki katika maadhimisho hayo ambapo shughuli mbalimbali zenye mnasaba na tukio hilo zilifanyika.

***56.*** **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilifanikisha kufanyika kwa Kongamano la Saba la Kiswahili la Kimataifa lililowajumuisha wadau na wanataaluma wa Kiswahili **258** kutoka ndani na nje ya nchi. Kauli mbiu katika Kongamano hilo ilikuwa ni ***"Kiswahili ni zaidi ya Lugha Tukitumie Kuimarisha Diplomasia".***

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Baraza la Kiswahili Zanzibar limefanikiwa kuzindua Jarida maalum la Kongamano na kuuza jumla ya machapisho **312** kwa njia kawaida na mtandao. Machapisho yaliyouzwa ni Kamusi la Kiswahili Fasaha, Kamusi la Lahaja ya Kitumbatu, Kamusi la Lahaja ya Kipemba, Kamusi la Lahaja ya Kimakunduchi, Jarida la Jahazi, Kitabu cha Mawasiliano ya Msingi ya Kiswahili kwa Wageni, kitabu cha Dkt. Shein na Maendeleo ya Kiswahili na kitabu cha Utamaduni wa Mzanzibari kwa lengo la kuongeza mapato Serikalini.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia mkakati maalum wa kukibidhaisha Kiswahili duniani, BAKIZA limeendelea kutoa taaluma juu ya matumizi fasaha na sanifu ya Lugha ya Kiswahili. Katika

harakati hizo, jumla ya vipindi 66 vya Lugha ya Kiswahili vimerushwa hewani kupitia vituo 17 vya TV na Redio vya ndani na Nje ya Nchi. Aidha, vibango 145 vimerushwa kupitia mitandao ya kijamii kwa lengo la kutoa taaluma na kutangaza machapisho ya BAKIZA.

***59.*** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza la Kiswahili imeendelea kuhariri nyaraka mbalimbali kutoka lugha za kigeni kuenda lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwawezesha waswahili kusoma na kuzifahamu nyaraka hizo. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2024, jumla ya nyaraka 6 zimetafsiriwa kwenda katika Lugha ya Kiswahili. ***Kiambatisho nambari 4A kinahusika.***

**60. MheshimiwaSpika,**katikakukuzanakuimarisha Michezo, Serikali imeziwezesha Timu za Taifa kushiriki katika mashindano ya CECAFA ya mpira wa miguu kwa vijana wenye umri chini ya miaka 15 (U-15) yaliyofanyika Uganda na chini ya miaka 18 (U-18) yaliyofanyika Kenya. Timu ya vijana walio chini ya umri wa miaka 15 waliibuka mshindi wa kwanza na wenzao wenye umri chini ya miaka 18 walifika hatua ya makundi. Hatua hiyo muhimu imeongeza hamasa kubwa kwa viongozi wa Serikali, wananchi, na wanamichezo kwa ujumla.

**61. Mheshimiwa Spika,** Chama Cha Netball cha Zanzibar na Chama Cha Netball cha Tanzania

Bara vimelipiwa ada ya mwaka ya uwanachama ili viweze kuendelea kutambulika Kikanda na Kimataifa. Sambamba na kutoa mafunzo ya uongozi kwa viongozi vijana **30** wanaoongoza michezo hapa Zanzibar. Mafunzo hayo yaliendeshwa na mtaalamu kutoka Ujerumani Dr. Angela, katika uwanja wa Mao Ze-dong mwezi Januari, 2024.

62. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, mashindano makubwa ya Kombe la Mapinduzi yalifanyika Zanzibar kuanzia Disemba 28, 2023 na kumalizika Januari 13, 2024. Jumla ya timu 5 kutoka Zanzibar, 4 kutoka Tanzania Bara na timu 3 kutoka nje ya Tanzania zilishiriki katika mashindano hayo. Timu ya Mlandege kutoka Zanzibar ilifanikiwa kutwaa ubingwa wa mashindano hayo kwa mwaka 2024 ikiwani mara ya pili mfululizo. Aidha, Serikali zetu mbili Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimefanikiwa kulirejesha Kombe la Muungano kwa mwaka 2024, kombe hilo lilishirikisha timu nne mbili kutoka Tanzania Bara na mbili kutoka Zanzibar ambapo mshindi wa mwaka 2024 ni Simba Sports Club.

63. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Sera ya michezo ya mwaka 2018, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imefanikiwa kusimamia mashindano mbali mbali yaliyoshirikisha timu

kutoka kwenye Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali. Michezo iliyoshindaniwa ni mpira wa miguu, kuvuta kamba na Netball ambapo kwa upande wa mchezo wa mpira wa miguu timu 24 ziliweza kushiriki Unguja na timu 8 zilishiriki Pemba.

64. **Mheshimiwa Spika,** Bingwa wa mashindano ya mpira wa miguu kutoka Unguja alicheza na bingwa kutoka Pemba katika uwanja wa New Amaan Complex ili kupata mshindi wa jumla. Hatimae timu ya Bandari kutoka Pemba ilifanikiwa kutwaa ubingwa kwa mwaka 2024. Kwa upande wa mashindano ya kuvuta kamba timu 2 zileweza kushiriki na timu ya bandari ya Unguja ilifanikiwa kuwa mshindi. Vile vile, kwa mashindano ya netball timu 2 zilishiriki na timuya bandari ya Unguja ilifanikiwa kuwa bingwa wa mashindano hayo. Lengo la mashindano hayo ni kuzidisha hamasa miongoni mwa wachezaji na wafanyakazi kwa kuongeza ushirikiano, udugu na umoja miongoni mwao na taasisi zao.

65. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuinua michezo, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar alishiriki katika Tamashala siku ya mazoezi ya viungo Kitaifa lililofanyika katika uwanja wa Amaan, tarehe 1 Januari, 2024. Jumla ya vilabu **173** vilishiriki, kati ya hivyo vilabu **100** kutoka Unguja, **25** kutoka Pemba na

vilabu **48** kutoka Tanzania Bara ambapo zaidi ya wanamazoezi **5,000** walishiriki. Kauli mbiu katika Tamasha hilo kwa mwaka 2024, ilikua ni ***"Fanya mazoezi Imarisha Afya yako, Tunza Mazingira linda Maisha yako".***

***66.*** **Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kuviunga mkono vyama vya michezo Zanzibar, Serikali imevisaidia vyama vinne (4) vya michezo kuandaa na kushiriki mashindano ya Kikanda na Kimataifa. Vyama hivyo viliweza kuiwakilisha Zanzibar kimichezo kwenye mashindano yaliyofanyika ndani na nje ya nchi. Sambamba na hilo, Serikali imevisaidia vyama 7 kufanya uchaguzi. Lengo ni kuleta usawa, kuendeleza amani, upendo na ushirikiano katika michezo. ***Kiambatisho nambari 5A kinahusika***

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar imepata fursaya kuwa mwenyeji wa mashindano makubwa ya mpira wa miguu Afrika yanayoitwa CAF African Schools Football Championship. Ni mashindano yaliyozikutanisha timu 14 (timu saba za Wanaume na timu saba za Wanaweke) za vijana wenye umri wa chini wa miaka 15 kutokaMataifa mbali mbali Afrika. Mashindano haya yalianza mwaka jana nchini Afrika Kusini na mwaka huu umefanyika Uwanja wa New Amaan Complex, kuanzia tarehe 21 Mei hadi tarehe 24 Mei 2024. Mbali na mashindano hayo CAF waliendesha mafunzo ya leseni D ya Grassroot,

yaani makocha wa wachezaji wadogo, Waandishi wa Habari wadogo, Afya yaani safeguarding na usalama kwenye michezo yaani security.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

68. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uimarishaji wa viwanja vya michezo unatekelezwa ndani ya programu ndogo ya uendeshaji na ukuzaji wa michezo. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa kutumia **shilingi 34,278,054,000/-** Kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za ujenzi wa viwanja vya wilaya na ukarabati wa viwanja vya michezo. Hadi kufikia mwezi machi 2024, jumla ya **shilingi 31,709,606,872/-** sawa na **asilimia 92.5** zimepatikana.

69. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikisha Ukarabati wa viwanja viwili vikubwa, kiwanja cha Amaan Unguja na kiwanja cha Gombani Pemba kwa mafanikio makubwa. Lengo la kuifanyia ukarabati Miundombinu hiyo ya Michezo ni kuiboresha ili iwe na muonekano wa kisasa na iweze kutumika katika mashindano ya Kikanda na Kimataifa.

70. **Mheshimiwa Spika,** Mradi mwengine uliotekelezwa ni mradi wa ***"Sports for Development in Africa"*** ambao unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la GIZ kutoka Ujerumani.

Lengo la mradi huu ni kuweka usawa wa kijinsia na kushirikisha Watu Wenye Ulemavu katika masula ya michezo. Mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 3 kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2025 ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2023 shughuli ya upimaji wa viwanja na kutangaza zabuni zimefanyika. Kupitia mradi huu jumla ya viwanja vitano vya michezo midogo midogo (3 in 1) vitajengwa na viwanja vitatu vitakarabatiwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Maeneo yaliyofanyiwa vipimo kwa ajili ya ujenzi yanaonekana kwenye ***kiambatisho nambari 5B.***

**Programu ya Uendeshaji na Mipango Katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**

**71.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii iliidhinishiwa jumlaya **shilingi 3,542,926,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2024 jumlaya **shilingi 2,315,186,214/-** sawa na asilimia 65 zimepatikana. ***Kiambatisho Nambari 1A kinahusika.***

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi na vifaa mbali mbali vya kazi kwa ajili ya kuongeza bidii na kuimarisha ufanisi wa kazi. Pia, wafanyakazi wote wamepatiwa stahiki zao kama vile malipo baada ya saa za kazi, huduma ya likizo, malipo

ya ufiwa, malipo ya safari kikazi na likizo la uzazi. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano na Mpango wa manunuzi wa mwaka 2023/2024.

73. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kukuza na kuimarisha utendaji wa kazi, Wizara imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi **60** (31 wanawake na 29 wanaume) na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi **193** (wanawake 105 na wanaume 88) katika ngazi na fani tofauti. Mafunzo yote haya yalilenga kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu ya wafanyakazi ya kila siku.

74. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ndogoya Utawala na Uendeshaji, kumekuwa na usimamizi mzuri wa ziara za kikazi za Viongozi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara. Lengo la ziara hizi ni kufuatilia na kusimamia kwa ukaribu shughuli za Wizara na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili watendaji na taasisi. Aidha, watendaji wakuu wa Wizara wamewezeshwa kushiriki mikutano mbali mbali nje ya nchi ikiwemo Kenya, Botswana, Uganda, Ujerumani, India na China kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na wadau waliopo nje ya nchi. Vile vile, Wizara imewaombea vibalivya kazi watumishi **23** wa kigeni kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa miradi na programu za Wizara.

75. **Mheshimiwa Spika,** ili kuleta ufanisi mzuri wa matumizi ya rasilimali fedha, Wizara imeweza kufanya ukaguzi wa ndani na kutoa ripoti za fedha na ukaguzi kwa kila robo mwaka kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma yanafanyika. Aidha, Wizara imeratibu mikutano mbalimbali ya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi, mikutano ambayo imeweza kuongeza ufanisi na kasi kubwa katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara. Pia, kupitia kitengo cha Habari na Mawasiliano, Wizara imeweza kurusha hewani habari na matukio mbalimbali kupitia mitandao ya kijamii kama vile *facebook, Instagram, whatsapp* pamoja na *Website* ya Wizara.

76. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii, Wizara imefanikiwa kutayarisha Mpango wa Mwaka wa Utekelezaji, Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini na kutayarisha na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika taasisi zinazo husika. Aidha, imetayarisha hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

77. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005 na Sera ya Habari ya mwaka 2005 na kuzindua Sera mpya za mwaka 2023. Aidha, Rasimu ya Sera ya Utamaduni na Sera ya Utangazaji zimeshakamilika kwa ngazi ya Wizara na zinatarajiwa kuwasilishwa katika

vikao vya Makatibu Wakuu na vikao vya Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kupata maoni na kutolewa maamuzi. Vile vile, utayarishaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Sera hizo unaendelea kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa Sera.

78. **Mheshimiwa Spika,** utafiti mdogowa uanzishwaji wa mchezo wa kuteleza magari (Car drafting) umefanyika. Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huo **asilimia 86.8** ya watoa maoni wamewafiki kuanzishwa kwa mchezo huo kutokana na fursa mbalimbali ikiwemo ajira kwa vijana. Aidha, Wizara imeandaa waraka ambao utawasilishwa Serikalini kwa ajili ya kutolewa maamuzi.

79. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa miradi, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo Unguja na Pemba. Miradi iliyofuatiliwa ni Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Amaan na Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani Pemba katika programu ya Ujenzi na Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. Vile vile, maafisa 12 walipatiwa mafunzo ya usimamizi wa miradi kwa lengo la kuwawezesha kuwa na ufanisi katika usimamizi, ufuatiliaji na udhibiti wa Miradi.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Wizara imefanikisha kufanyika vikao vitatu vya kiutendaji vya Maafisa Mipango

wa taasisi zilizo chini ya Wizara. Kupitia vikao hivyo, maelekezo juu ya utayarishaji wa ripoti, uandaaji wa mipango na usimamizi wa Programu yalitolewa. Kadhalika, Wizara imeendelea kuratibu ziara za Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii, Kamati ya Bajeti na Kamati ya PAC Unguja, Pemba na Dar- es- Salaam katika kufanya ufuatiliaji wa shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara.

81. **Mheshimiwa Spika,** shughuli nyengine iliyotekelezwa kwa mafanikio ni maafisa watatu kushiriki katika vikao tofauti vya ushirikiano vilivyofanyika Dodoma na Dar es Salaam. Vikao hivyo vilikuwa katika ngazi ya wataalamu vilivyojadili ushirikiano baina ya Tanzania na Ethiopia, Tanzania na China na Tanzania na Angola. Lengo la vikao hivyo ni kuboresha uhusiano wa Kidiplomasia katika maeneo mbali mbali ya kiutendaji baina ya Tanzania na nchi za nje.

82. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii, Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kuratibu shughuli za Wizara kwa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani, kuratibu na kusimamia shughuli za habari, kusimamia shughuli za Michezo, kusimamia na kufuatilia programu mbalimbali za maendeleo ya vijana, kusimamia tamasha la 28 la Utamaduni wa Mzanzibari pamoja na kusimamia shughuli za sanaa na wasanii kwa upande wa Pemba.

83. **Mheshimiwa Spika,** Uwezo wa wafanyakazi umeendelea kuimarika na wenye kuleta ufanisi zaidi kutokana na kuendeleza programu za kujenga uwezo wao kitaaluma kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kulingana na mahitaji. Wafanyakazi watatu wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada ya uzamili katika fani ya ufuatiliaji na tathmini na stashahada ya Utunzaji wa kumbukumbu na rasilimali watu na wafanyakazi watano walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katikafani ya udereva, usafirishaji na utunzaji wa kumbukumbu. Sambamba na kuwapatia wafanyakazi taaluma ya namna ya kujikinga na maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

84. **Mheshimiwa Spika,** watendaji wa Ofisi Kuu Pemba wamefanya vikao mbalimbali vya wafanyakazi na vikao vya Kamati Tendaji kwa lengo la kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Serikali na kukumbushia haki na wajibu wa kila mfanyakazi. Aidha, Ofisi kuu Pemba imeweza kuratibu vikao na ziara za Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakili, zikiwemo kutembelea Kituo cha Mafunzo ya Vijana Weni na Mradi wa Baraza la Vijana Wilaya ya Wete zimefanyika.

85. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira bora ya kazi, Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kutoa huduma za kiutawala na za kiendeshaji

kwa kuwapatia wafanyakazi vifaa na vitendea kazi vya ofisi. Aidha, wafanyakazi wamepatiwa stahiki zao muhimu ikiwemo malipo ya muda wa saa za ziada wafanyakazi 8, huduma ya likizo wafanyakazi 17, malipo ya safari kikazi wafanyakazi 10, na ubani wa ufiwa wafanyakazi 5 Ofisi inaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo, mpango wa manunuzi na mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano.

## E. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

86. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imeandaa bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa mujibu wa muongozo wa utayarishaji wa bajeti ya Serikali. Aidha, Wizara imeongezewa fungu jipya na hivyo kuifanya kuwa na mafungu mawili ambayo ni Fungu J03 la Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Fungu J05 kwa ajili ya Tume ya Utangazaji Zanzibar. Pia, Wizara inaendelea kutekeleza shughuli zake kupitia Programu Kuu 4 na Programu ndogo 8.

87. **Mheshimiwa Spika,** bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imeongezeka kwa **bilioni 2,890,220,000/-** sawa na asilimia 16 ya ongezeko la matumizi ya kazi za kawaida. Kutoka **bilioni 17,661,930,000/-** mwaka 2023/2024 hadi **bilioni 20,552,150,000/-** mwaka 2024/2025. Kwa miradi ya maendeleo ongezeko

ni **bilioni 35,945,928,000/-** sawa na **asilimia 105** Kutoka **bilioni 34,278,054,000/-** mwaka 2023/2024 hadi **bilioni 70,223,982,000/-** mwaka 2024/2025. Ongezeko hili ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bajeti ya kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. ***Kiambatisho nambari 1E kinahusika***

88. **Mheshimiwa Spika,** katika Fungu J03 fedha za nyongeza kwa upande wa kazi za kawaida zimeelekezwa katika ununuzi wa jenereta la Ofisi, kusaidia Timu za Taifa kushiriki Mashindano ya Kikanda na Kimataifa, Kuandaa Mashindano ya Kikanda na Kimataifa na Kuimarisha Mazingira bora ya Kazi. Katika miradi ya Maendeleo fedha za nyongeza zimeelekezwa katika kufanikisha shughuli za ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Viwanja vya Michezo katika eneo la Maisara.

89. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fungu J05 bajeti imeelekezwa kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo ununuzi wa gari la kufuatilia Mwenendo wa Matumizi ya Masafa ya Utangazaji, Ununuzi wa Gari la Ofisi ya Tume ya Utangazaji Pemba na Kuimarisha mazingira bora ya kazi.

90. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imejipangia kutekeleza vipaombele vifuatavyo:-

i. Kusimamia masuala ya habari na utangazaji kwa kuzijengea uwezo Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji na kununua vitendea kazi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya habari;

ii. Kuimarisha Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na Kampuni ya ZMUX kwa kuzipatia vifaa, wataalamu na miundombinu imara ya kurushia matangazo ili ziweze kutayarisha na kurusha hewani vipindi vyenye ubora;

iii. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika vyombo vya habari ili kutanua wigo wa upatikanaji wa habari kwa wananchi mijini na vijijini;

iv. Kuimarisha uwezo wa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kwa kuongeza nakala za magazeti yanayochapishwa na kuhakikisha yanasambazwa kwa wakati nchi nzima. Sambamba na kuliuza gazeti kwa njia ya mtandando ili lisomwe duniani kote;

v. Kuimarisha uwezo wa Wakala wa Uchapaji Zanzibar kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vya uchapaji, malighafi na kuimarisha huduma za bohari kuu ya Serikali;

vi. Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya vijana nchini, kuwawezesha vijana na kuwajengea uwezo ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa;

**vii.** Kuandaa na kutekeleza programu za elimu na malezi, utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa vijana pamoja na mikakati ya kujenga moyo wa uzalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao;

**viii.** Kuendeleza, kukuza na kueneza Kiswahili na kuwa bidhaa katika matumizi ya shughuli za taaluma zikiwemo za uandishi, uchapishaji, ukalimani na kuwa moja ya lugha iliyo rasmi inayozungumzwa na kutambulika katika mashirika na mikutano ya Kikanda na Kimataifa;

